BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

FOMATI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION – PSLE)

IMETOLEWA NA:
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P. 2624
DAR ES SALAAM
TANZANIA

JANUARI, 2011

YALIYOMO

UTANGULIZI iv
01 LUGHA YA KISWAHILI 1
02 ENGLISH LANGUAGE 5
03 MAARIFA YA JAMII 8
04 HISABATI 14
05 SAYANSI 17

UTANGULIZI

Fomati hii mpya ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi imeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya mtaala wa Elimu ya Msingi yaliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi **mwaka 2005** na kuanza kutumika **mwaka 2007.** Aidha fomati hii imezingatia mabadiliko ya msingi ya utoaji wa mtihani wenye mtazamo wa mhamo wa ruwaza kwa kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya upimaji uliolenga mtahiniwa katika kumudu maudhui ya mada zilizoainishwa kwenye mihutasari ya masomo yanayofundishwa katika shule za msingi. Mtihani utapima pia jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla.

Masomo yaliyotahiniwa katika mtaala uliokuwepo ni pamoja na Lugha ya Kiswahili, English Language, Maarifa ya Jamii, Hisabati na Sayansi. Somo la Stadi za Kazi limekuwa likifundishwa katika shule za msingi ingawa halikutahiniwa Kitaifa. Katika mtaala mpya masomo yameongezeka kutoka **sita** hadi **masomo kumi na moja** kama ilivyobainishwa katika Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2006 wenye **Kumb. Na. ED/ CK/C.2/4/V/2** wa **tarehe 04/04/2006**. Masomo ya lazima ni Lugha ya Kiswahili, English Language, Uraia, Historia, Jiografia, Stadi za Kazi, Hisabati, Sayansi na Haiba na Michezo. Aidha masomo ya kuchagua ni pamoja na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Lugha ya Kifaransa. Masomo mapya ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Haiba na Michezo, Lugha ya Kifaransa na masomo ya Dini.

Masomo yatakayotahiniwa kuanzia **mwaka 2011** ni Lugha ya Kiswahili, English Language, Maarifa ya Jamii (Uraia, Historia na Jiografia), Hisabati na Sayansi. Masomo hayo yatatahiniwa kwa muda wa **siku mbili**. Masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo, TEHAMA, French Language na masomo ya Dini yataendelea kufundishwa katika shule za msingi ingawa hayatatahiniwa Kitaifa.

Fomati hii imeandaliwa kwa kuzingatia mada zilizomo katika mihutasari mipya inayofundishwa katika Shule za Msingi ili kutoa mwongozo kwa walimu na wanafunzi kuhusu muundo wa mtihani. Walimu na wanafunzi wanashauriwa kutotumia fomati hii kama mbadala wa mihutasari. Katika

ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mada zote zilizoainishwa katika mihutasari ya shule za msingi zifundishwe kikamilifu.

Fomati ya kila somo inaonesha Utangulizi, Malengo ya Jumla, Ujuzi wa Jumla, Muundo wa Mtihani na Mada zitakazotahiniwa. Muda wa kufanya mtihani kwa kila somo umeoneshwa. Watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu wataongezewa muda wa ziada wa kufanya mtihani wa dakika 10 kwa kila saa kwa masomo ya lugha, sanaa na sayansi na dakika 20 kwa kila saa katika somo la Hisabati.

Baraza la Mitihani linatoa shukurani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu na Walimu wa Shule za Msingi walioshiriki katika kuandaa fomati hii. Aidha Baraza la Mitihani litakuwa tayari kupokea ushauri, maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau wa elimu kuhusu fomati hizi kwa lengo la kuziboresha.

A. J.M. Kitali
Kny: Katibu Mtendaji
Baraza la Mitihani la Tanzani

01 LUGHA YA KISWAHILI

1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Lugha ya Kiswahili inatokana na Muhtasari wa somo la Lugha ya Kiswahili wa mwaka 2005 ulioanza kutumika Januari 2007. Muhtasari huo uliboreshwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mtaala.

Aidha fomati hii mpya ya mtihani wa Lugha ya Kiswahili imetofautiana na ile ya mwaka 2005 kwa sababu imeingiza mabadiliko ya msingi ya utoaji mtihani wenye kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika upimaji wa namna mtahiniwa alivyomudu maudhui za mada mbalimbali zilizoainishwa kwenye muhtasari. Mtihani utapima pia jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika jamii ili kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa jumla.

2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa Lugha ya Kiswahili unalenga katika kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kutumia Kiswahili fasaha katika hali na miktadha mbalimbali kwa kuzungumza, kusoma na kuandika.

2.2 kutumia lugha ya Kiswahili katika kupata maarifa, stadi na mienendo ya kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.

2.3 kuwasiliana kwa kutumia sarufi ya Kiswahili Sanifu.

2.4 kutumia lugha ya kisanii katika miktadha mbalimbali.

2.5 kupata misingi bora na imara na kujifunza kwa ajili ya kujiendeleza.

2.6 kuthamini Kiswahili kama ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

3.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani unalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 kuzungumza na kuandika Kiswahili kwa ufasaha ili kukidhi mahitaji ya msingi ya mtumiaji wa lugha ya Kiswahili.

3.2 kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili katika shughuli za kila siku katika miktadha na mazingira mbalimbali.

3.3 kusoma na kuandika sentensi, habari fupi na ndefu.

3.4 kukipenda na kukithamini Kiswahili kama lugha ya Taifa na ya Kimataifa.

3.5 kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano.

3.6 kujisomea maandiko ya kiada na ziada kwa ufahamu, kupata maarifa na kwa burudani.

4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani wa Kiswahili utakuwa na sehemu A, B, C, D na E. Sehemu A itahusisha mada ya Sarufi, sehemu B itahusisha mada ya Lugha ya Kifasihi, sehemu C itahusisha mada ya Ufahamu, sehemu D itahusisha mada ya Ushairi na sehemu E itahusisha Utungaji au Uandishi.

4.2 Mtihani utakuwa na jumla ya maswali **hamsini (50)** na watahiniwa watatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.3 Muda wa kufanya mtihani utakuwa saa **1:30** ambapo watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu watafanya mtihani kwa muda wa saa **1:45**.

4.4 Kila swali litakuwa na alama **moja (1)**.

4.5 SEHEMU A: Sarufi

4.5.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **ishirini (20)** ya

kuchagua. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote.

4.5.2 Maswali katika sehemu hii yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.5.3 Maswali yatajikita katika kubainisha aina za maneno, kutumia kwa usahihi aina mbalimbali za maneno, miundo ya sentensi na nyakati mbalimbali.

4.6 SEHEMU B: Lugha ya Kifasihi

4.6.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi (10)** ya kuchagua. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote.

4.6.2 Maswali katika sehemu hii yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.6.3 Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.6.4 Maswali yatajikita katika mada ya methali, nahau na vitendawili.

4.7 SEHEMU C: Ufahamu

4.7.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi (10)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote.

4.7.2 Maswali yote yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.7.3 Maswali yatajikita katika ufahamu wa kusoma habari, vipengele vya kifasihi na matumizi ya kamusi.

4.8 SEHEMU D: Ushairi

4.8.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **sita (6)** ya kuchagua jibu lililo sahihi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote.

4.8.2 Maswali katika sehemu hii yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.8.3 Maswali hayo yatajikita zaidi katika mada ya ushairi na tenzi.

4.9 SEHEMU E: Utungaji/Uandishi wa Habari na Barua

4.9.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **manne (4)** ambayo majibu yake yanakamilisha kifungu cha habari chenye mtiririko unaoleta maana.

4.9.2 Maswali haya yatakuwa ya kuchagua sentensi sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.9.3 Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote.

5.0. MADA ZITAKAZOTAHINIWA

5.1 Sarufi

5.2 Lugha ya kifasihi

5.3 Ufahamu

5.4 Ushairi

5.5 Utungaji/Uandishi wa barua/Habari

02 ENGLISH LANGUAGE

1.0 INTRODUCTION

This examination format is based on English Language syllabus of 2005 which was effected to teaching for the first time on January 2007. The English Language syllabus was prepared by considering the changes of paradigm shift from content to competence based which were effected in the curriculum.

Furthermore, the new examination format aims at assessing candidates' competences, skills and attitudes in response to paradigm shift in learning and assessing candidates rather than assessing the candidates ability to master the content as stipulated in the syllabus. The examination will also assess how candidates use the attained competences in solving social, political, economic and technological advances for the betterment of his/her development and the nation at large.

2.0 GENERAL OBJECTIVES

The English examination aims at testing candidates' ability to:

2.1 read and comprehend the passage given.

2.2 answer the questions based on the passage.

2.3 use English grammar correctly.

2.4 use English language correctly in a given situation.

2.5 write letters and composition.

3.0 GENERAL COMPETENCES

The examination will measure the candidate's competences on how to:

3.1 use basic expression to satisfy his/her basic needs.

3.2 communicate by using English language in different contexts.

4.0 EXAMINATION RUBRIC

4.1 The English language examination consists of sections A, B, C and D. Section A will comprise of Grammar, Section B Vocabulary, Section C Composition and Section D Comprehension. Each question will carry **1 mark**.

4.2 The examination paper will have a total number of **fifty (50)** questions.

4.3 Candidates will be required to answer **all** questions.

4.4 The paper will consist of **1:30 Hours**. Visual impaired and low vision candidates will consists of **1:45 Hours**.

4.5 Each question consists of **one** (**1**) mark.

4.6 SECTION A: Grammar

4.6.1 This section will consist of **thirty (30)** questions of which **ten** (**10**) questions will be set from Tenses topic and 20 questions from other forms of grammar.

4.6.2 Candidates will be required to answer **all** the questions.

4.6.3 The section will comprise multiple choice questions. The correct answer will be chosen from options A, B, C, D na E.

4.6.4 SECTION B: Vocabulary

4.6.5 This section will consist of **six (6)** multiple choice questions.

4.6.6 Candidates will be required to answer **all** the questions.

4.6.7 The correct answer will be chosen from options A, B, C, D na E.

4.7 SECTION C: Composition

4.7.1 This section will comprise **four** (**4**) multiple choice questions of which the answers will form a composition in a logical order.

4.7.2 The correct sentence in each question will be chosen from options A, B, C, D na E.

4.7.3 Candidates will be required to answer **all** the questions.

4.8 SECTION D: Comprehension

4.8.1 This section will consist of a short passage which will be followed by **ten (10)** multiple choice questions.

4.8.2 Candidates will be required to answer **all** the questions.

4.8.3 The correct answer will be chosen from options A, B, C, D and E.

5.0 TOPICS TO BE EXAMINED

5.1 Tenses

5.2 Other forms of Grammar

5.3 Vocabulary

5.4 Composition

5.5 Comprehension

03 MAARIFA YA JAMII

(HISTORIA, URAIA NA JIOGRAFIA)

1.0 UTANGULIZI

Fomati hii mpya ya Maarifa ya Jamii inatokana na mihutasari ya masomo ya Historia, Uraia na Jiografia ya mwaka 2006 iliyoanza kutumika Januari 2007. Mihutasari hiyo iliyoboreshwa ilitungwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mtaala.

Fomati hii mpya ya mtihani imetofautiana na ile ya mwaka 2005 kwa sababu imeingiza mabadiliko ya msingi ya kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya mkazo katika kupima maudhui ya mada zilizotajwa katika mihtasari. Kila somo katika fomati hii limepewa uzito unaostahili katika muundo wa mtihani. Hivyo somo la Maarifa ya Jamii litakuwa na karatasi moja ya mtihani ambayo itahusisha masomo matatu.

Mtihani utapima jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika jamii kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla.

2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa Maarifa ya Jamii (Historia, Uraia na Jiografia) unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kuelewa chimbuko la binadamu, mabadiliko yake kimaumbile na maendeleo yake kijamii na kiteknolojia.

2.2 kufahamu jinsi mambo yaliyopita yanavyoathiri mambo ya sasa na yajayo.

2.3 kuelewa matatizo yaliyosibu na yanayosibu jamii za Kitanzania na jamii za majirani na jinsi yanavyotatuliwa.

2.4 kutambua na kuthamini utamaduni wa Taifa na wa jamii nyingine pamoja na kujenga na kutekeleza misingi ya utamaduni unaofaa.

2.5 kutambua jinsi mahusiano baina ya jamii za Kitanzania na za mataifa mengine yalivyoathiri maendeleo ya Tanzania.

2.6 kukuza stadi za kutumia vyanzo mbalimbali vya Historia ili kupata maarifa na kuyatumia.

2.7 kuelewa misingi ya demokrasia katika shughuli za utawala na uongozi wa asasi au taasisi zinazohusika.

2.8 kuthamini, kuheshimu na kutetea Katiba ya nchi na utawala wa kidemokrasia.

2.9 kuelewa na kushiriki katika Ulinzi na Usalama wa Taifa.

2.10 kutambua muundo wa uongozi wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

2.11 kuwa na uwezo wa kuchambua masuala mtambuka na athari zake katika njia endelevu kwa kutumia teknolojia sahihi.

2.12 kuelewa rasilimali zilizopo kwenye mazingira yake na kujenga mwelekeo chanya katika kuzitumia ili kuleta maendeleo yake binafsi na ya jamii nzima.

2.13 kubainisha maendeleo muhimu ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisayansi na kiteknolojia ambayo jamii ya kitanzania inashirikiana na mataifa mengine kuyaendeleza.

3.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani unalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 kuchanganua taarifa za chimbuko la binadamu katika nyakati mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto za maendeleo.

3.2 kuchambua mila na desturi katika jamii na kuziendeleza zile zinazofaa kwa ajili ya kujenga heshima, utu wa mwafrika na uzalendo.

3.3 kupenda kujisomea maandiko mbalimbali, kutafsiri matukio na mabaki ya kihistoria kiushirikeni na kiyakinifu ili kuweza kuyahifadhi na kuyatumia katika kukuza sekta ya utalii na kujiendeleza kitaaluma.

3.4 kutafuta, kuchambua, kutafsiri na kutumia kwa ufanisi taarifa za kihistoria ili ziwawezeshe watahiniwa kujenga na kutetea hoja.

3.5 kuwa na uwezo wa kuthamini na kushiriki katika kujenga, kutetea hoja na kuonyesha msimamo thabiti unaohusu uongozi na serikali.

3.6 kuwa tayari kusaidia na kusuluhisha migogoro katika jamii husika.

3.7 kuonyesha utayari na ari ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia katika jamii husika na jamii nyingine.

3.8 kuwa na uwezo wa kubaini na kuchambua masuala mtambuka katika jamii na kuonesha misimamo sahihi.

3.9 kutumia teknolojia sahihi kutafuta, kuchambua na kutafsiri mazingira na hali ya kutegemeana, athari zake na kutumia maarifa hayo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

3.10 kutambua rasilimali zilizopo Tanzania na nchi nyingine kwa kushirikiana na mataifa mengine katika kutatua matatizo ya mazingira.

4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani wa Maarifa ya Jamii utakuwa na sehemu A, B na C. Sehemu A itahusisha mtihani wa Historia, sehemu B Uraia na sehemu C Jiografia.

4.2 Mtihani utakuwa na jumla ya maswali **hamsini (50).**

4.3 Mtahiniwa atatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.4 Muda wa kufanya mtihani utakuwa saa **1:30** ambapo watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu watafanya mtihani kwa muda wa saa **1:45**.

4.5 Kila swali litakuwa na alama **moja (1)**.

4.6 SEHEMU A: Historia

4.6.1 Mtihani wa Historia utakuwa na jumla ya maswali **18.**

4.6.2 Mtahiniwa atatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.6.3 Maswali katika sehemu hii, yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.7 SEHEMU B: Uraia

4.7.1 Mtihani wa Uraia utakuwa na jumla ya maswali **14**.

4.7.2 Mtahiniwa atatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.7.3 Maswali katika sehemu hii, yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.8 SEHEMU C: Jiografia

4.8.1 Mtihani wa Jiografia utakuwa na jumla ya maswali **18**.

4.8.2 Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.8.3 Maswali katika sehemu hii, yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

5.0 MADA ZITAKAZOTAHINIWA

Mada zitakazopimwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ni kama ifuatavyo:

5.1 HISTORIA

5.1.1 Elimu ya familia

5.1.2 Chimbuko na mabadiliko ya binadamu

5.1.3 Mahusiano ya Watanzania na jamii za kigeni

5.1.4 Tanzania huru

5.1.5 Uvamizi wa kimataifa

5.1.6 Afrika huru

5.2 URAIA

5.2.1 Uongozi

5.2.2 Alama za shule na za taifa

5.2.3 Misingi ya demokrasia

5.2.4 Ulinzi na usalama

5.2.5 Utamaduni wetu

5.2.6 Uchumi wetu

5.2.7 Ushirikiano baina ya Tanzania na mataifa mengine

5.3 JIOGRAFIA

5.3.1 Mazingira

5.3.2 Picha

5.3.3 Ramani

5.3.4 Usomaji wa ramani

5.3.5 Mfumo wa Jua

5.3.6 Majanga

5.3.7 Maji

04 HISABATI

1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Hisabati inatokana na Muhtasari wa somo wa mwaka 2005 ulioanza kutumika Januari 2007. Muhtasari huo ulioboreshwa ulitungwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mtaala.

Aidha fomati hii mpya ya mtihani imetofautiana na ile ya mwaka 2005 kwa sababu imeingiza mabadiliko ya msingi ya kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika kupima maudhui ya mada mbalimbali zilizoainishwa katika muhtasari. Mtihani utapima pia jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika jamii kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa jumla.

2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani wa Hisabati unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kutumia stadi na ujuzi wa Hisabati alioupata ili kurahisisha utendaji wa shughuli mbalimbali za kielimu, kijamii, kiuchumi na kiufundi.

2.2 kutumia maarifa, mantiki na stadi za Hisabati kwa ajili ya maendeleo yake na ya jamii.

3.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa Hisabati utapima ujuzi na stadi alizopata mtahiniwa katika:

3.1 kutambua na kufanya matendo ya Hisabati.

3.2 kuchora, kuwasilisha na kutafsiri data, takwimu na grafu.

3.3 kutambua na kufumbua mafumbo kwa kukokotoa, kukadiria, kupanga, kuorodhesha, kufafanua, kuainisha na kurahisisha.

3.4 kufumbua kwa kupima, kuunda na kutengeneza vifaa (violwa na modeli sahihi) vya Hisabati.

3.5 kutumia stadi za kihisabati katika maendeleo yake na jamii kwa jumla.

4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani wa Hisabati utakuwa na sehemu A, B na C.

4.2 Sehemu A itahusisha namba na matendo ya kihisabati, Sehemu B itahusisha maswali ya maumbo na Sehemu C itahusisha maswali ya mafumbo.

4.3 Mtihani utakuwa na jumla ya maswali **hamsini (50)** na watahiniwa watatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.4 Muda wa kufanya mtihani utakuwa saa **1:30** ambapo watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu watafanya mtihani kwa muda wa saa **1:45**.

4.5 Kila swali litakuwa na **alama 1**.

4.6 SEHEMU A: Matendo ya Kihisabati

4.6.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **ishirini na tano (25)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.6.2 Maswali hayo yatahusu namba na matendo ya kihisabati.

4.6.3 Mtahiniwa atatakiwa kukokotoa na kisha kuchagua jibu lililo sahihi katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.7 SEHEMU B: Maumbo

4.7.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi na tatu**

(13) na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.7.2 Maswali hayo yatahusu maumbo.

4.7.3 Mtahiniwa atatakiwa kukokotoa na kisha kuchagua jibu lililo sahihi katika chaguzi A, B, C, D na E.

4.8 SEHEMU C: Mafumbo

4.8.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi na mbili (12)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.8.2 Maswali hayo yatahusu mafumbo.

4.8.3 Mtahiniwa atatakiwa kukokotoa na kisha kuchagua jibu lililo sahihi katika chaguzi A, B, C, D na E.

5.0 MADA ZITAKAZOTAHINIWA

5.1 Namba nzima

5.2 Sehemu, Desimali na Asilimia

5.3 Namba kamili

5.4 Namba za Kirumi

5.5 Vipimo

5.6 Majira ya Nukta

5.7 Takwimu

5.8 Algebra

5.9 Jometri

5.10 Fedha

5.11 Vipeo na vipeuo

05 SAYANSI

1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Sayansi inatokana na Muhtasari wa somo la Sayansi wa mwaka 2005 iliyoanza kutumika Januari 2007. Mihtasari hiyo iliyoboreshwa ilitungwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mtaala.

Aidha fomati hii mpya ya mtihani imetofautiana na ile ya mwaka 2005 kwa sababu imeingiza mabadiliko ya msingi ya kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika kupima namna mtahiniwa alivyomudu maudhui ya mada zilizoainishwa katika muhtasari. Mtihani utapima pia jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika jamii kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa jumla.

2.0 MALENGO YA JUMLA

Mtihani unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kuelewa na kutumia michakato ya Sayansi.

2.2 kubainisha na kutumia teknolojia kwa njia endelevu katika maisha ya kila siku.

2.3 kuelewa na kutumia maarifa na misingi ya Sayansi na Teknolojia.

2.4 kujenga mwelekeo chanya kuhusu Sayansi na Teknolojia.

3.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani utapima ujuzi alionao mtahiniwa katika:

3.1 kutambua hatua za mchakato wa uchunguzi wa kisayansi.

3.2 kubuni na kutumia ugunduzi wa kisayansi katika hali endelevu.

3.3 kutambua misingi ya Sayansi na kutumia Teknolojia kutatua matatizo ya jamii.

3.4 kupenda na kutumia misingi ya Sayansi na Teknolojia katika maisha ya kila siku.

4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani utakuwa na jumla ya maswali **hamsini (50).**

4.2 Mtahiniwa atatakiwa kufanya maswali **yote**.

4.3 Kila swali litakuwa na **alama moja (1)**.

4.4 Muda wa kufanya mtihani utakuwa saa **1:30** ambapo watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu watafanya mtihani kwa muda wa saa **1:45**.

4.5 Maswali yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C, D na E.

5.0 MADA ZITAKAZOTAHINIWA

5.1 Viumbe hai

5.2 Mahitaji muhimu kwa afya na uhai

5.3 Afya, huduma za afya na njia za kujikinga na magonjwa

5.4 Huduma ya kwanza

5.5 Virusi vya UKIMWI na UKIMWI

5.6 Mabadiliko ya Violwa, Hali na Matukio

5.7 Nishati, mashine na kazi

5.8 Mbinu na taratibu za kisayansi